

TOLEO LA VYOMBO VYA HABARI

## SAUTI YA MTAFSIRI



**Januari 30 - Mei 03, 2015**

.....

Wasanii: Sylvie Boisseau & Frank Westermeyer, Erik Bünger, Luis Camnitzer, Rainer Ganahl, Dora García, Joseph Grigely, Susan Hiller, Christoph Keller, Fabrice Samyn, Zineb Sedira, Mladen Stelinovic, Noline van Harskamp, Ingrid Wildi Merino

-

Mwangelizi: Martin Waldmeier  
Mshindi wa Tuzo la Wangelizi  
Wachanga 2014 MARCO/FRAC Lorraine/  
SFKM

-

Maonyesho yametolewa kwa kushirikiana na 49 Nord 6 Est - FRAC Lorraine, MARCO, Museo de Arte Contemporánea de Vigo, and Sogn og Fjordane Kunstmuseum

.....

[www.fracloorraine.org](http://www.fracloorraine.org)

Hivi leo, tafsiri ziko kila mahali: zinawezesha biashara ya bidhaa za kimataifa, zinawezesha majadiliano ya kidiplomasia kati ya viongozi wa kisiasa, kwa kukalimani matangazo ya habari zetu za kila siku, kuruhusu mawasiliano ya mtandaoni kati ya nchi na mabara, na kutujulisha kwa filamu na maandiko ya kigeni. Mengi tunayojua kuhusu ulimwengu yametufikia kupita tafsiri: kasi na uzito wa mawasiliano na mzunguko duniani unapoendelea kuchapuzwa, hitaji la tafsiri linaendelea kukua.

Tafsiri mara kwa mara uhusishwa na hasara. Baada ya yote, lugha na tamaduni sio njia tofauti ya kusema kitu kimoja, lakini njia tofauti za kusema mambo tofauti. Kwa hivyo tafsiri huwa ukadiriaji; kazi ngumu sana ya kuingia kati ya maonyesho tofauti ya uzofu wa mwanadamu. Kwa hivyo, tunawezaje kufikiria kuhusu makabiliano kati ya lugha kama siyo yenye changamoto na ngumu tu, bali kama chanzo cha ubunifu na mafunzo? Tunawezaje kuelewa ulimwengu kwa utofauti kwa lugha tofauti? Je, tafsiri inaweza kuwa mahali pa shughuli muhimu au hata ya uchochezi?

Kichwa cha mradi huu, «Sauti ya Mtafsiri», huelekeza kwa njia mbili za kiini. Kwa upande mmoja, hufipisha dhana ya kufanya shughuli ionekane - na sauti ya - tafsiri, na onyesho la kuiacha ichukue nafasi ya kati kama chanzo cha kipekee cha ufahamu kuhusu hali ya utofauti wa utamaduni. Kwa upande ule mwingine, umbo la mtafsiri huwa sitiari muhimu ya hali za lugha za utandawazi na enzi ya baada ya ukoloni: hitaji linalokuwa - na fucha, na uchungu - ili kujifunza lugha za kigeni; hali kujitolea au kutojitolea ya lugha mbalimbali za wahamiaji; makabiliano yaliyopo kati ya "lugha" za duniani na "tamaduni" za eneo lako; na tamaduni changamani na njia "zilizoangaziwa" za kuongea na kuona dunia.

Hivyo basi tafsiri sio kazi, au shughuli tu. Huwakilisha hali ya binadamu, na mara kwa mara, tunajipata tukichukua jukumu la mtafsiri

Martin Waldmeier  
London, 14.11.2014